
Jiandae leo maana kesho haitabiriki..., wekeza katika ufugaji kuku



Tunaishi majira mpya, **majira ya KUFANYA KAZI**, hivyo **yatupasa kufanya kazi**. Ikiwa upo katika ajira, basi hakikisha kuwa na wale wa nyumbani kwako **nao wanafanya kazi** zinazopelekea kuzalisha kipato.

SAYUNI POULTRY Gosheni tumekusudia kuelimisha wengine kile tulichojifunza, ili tuweze kwa pamoja kupiga hatua kimaendeleo kwa kutumia fursa katika ufugaji kuku.

Tunakushauri wewe binafsi (*bila kujali profesheno/ajira yako*), tumia muda wako binafsi (*sio wa kazi/ajira*) ukitumia simu '*smartphone*' yako au *'laptop'* yako katika kujifunza mambo muhimu ya maendeleo.

Baadhi yetu tupo kwenye ajira, lakini nyumbani tumeacha 'vijana wa kazi'(*maids*) ambao hawatumiki ipasavyo kiuchumi. **Kumbuka kuwa LEO wanakutegemea WEWE katika kujipatia kipato CHAO; lakini *huenda ikawa* kesho ukawategemea WAO katika kujipatia kipato CHAKO**. Hivyo basi LEO wahimize wao wafanye kazi, na **wewe ukiwajibika vilivyo katika ajira yako**. Huku wao wakiwa kama HAZINA (*assets*); na tena utumie eneo la kiwanja chako pia kama HAZINA (*assets*), wewe mwenyewe ukiwa MWEKEZAJI kwa kile ULICHONACHO LEO ajili ya KESHO yako na ya kwao. Kijana asiyefanya shughuli zenye manufaa kimaendeleo anakuwa ni mzigo/deni (***'liability'***) wakati anatakiwa kuwa hazina/msaada (***'asset'***). Hivyo basi **kwa kile ulicho nacho** "JIANDAE LEO MAANA KESHO HAITABIRIKI..., WEKEZA KATIKA UFUGAJI KUKU". **SAYUNI POULTRY Gosheni** tunasema ***"Thubutu na chukua hatua katika ufugaji kuku"***

Unaweza kututembelea kwenye mtandao **https://sayunipoultrygosheni.blogspot.com** au kwa kufika kwenye ofisi yetu Mbezi Mwisho. Pia uwe huru kwenda kwa '*Wafugaji Watotoleshaji*' wengine **waaminifu** uweze kupata kile unachohitaji katika kufanikisha kusudio lako katika ufugaji.

Na je unajua ?

- kuwa ni jambo la heshima kubwa unapoandaa kitoweo cha JOGOO (kuku) kwa ajili ya WAKWE (haswa ugeni wa baba mkwe/mama mkwe au ndugu au rafiki mpendwa) **kutoka bandani kwako mwenyewe** kuliko jogoo wa mtaa wa pili? ***"Thubutu leo"***
- kuwa nyama ya Kuku/ Khanga/Bata Mzinga ikiandaliwa kama '**nyama choma ya nyumbani**' (*a tantalized Home BBQ*) huleta umoja na upendo kwa familia na marafiki? ***"Thubutu leo"***
- kuwa maandalizi ya kufuga kuku wa kienyeji kwa ajili ya **mauzo ya Xmas na Mwaka mpya** ni sasa? ***"Thubutu leo"***
- kuwa Ufugaji wa Kuku (kienyeji) ni **mpenyo wa kiuchumi kwa wengine ambao wamekwama kabisa kimawazo wasijue wapi pa kuanzia** ? Usisite kuwajulisha, kwani **SAYUNI POULTRY Gosheni** tupo kwa ajili yao pia. ***"Nao waweze kuthubutu leo"***

Kwa nini usifuge leo ?

- ***"Thubutu leo kwa ajili ya kesho yako isiyotabirika"***
- Nasi **SAYUNI POULTRY Gosheni** tunasema "**UNAWEZA..,tena INAWEZEKANA**"

Kwa **WAFUGAJI waliopo kwenye UFUGAJI** tayari, hii ni fursa ya '*kujiongeza*' kwa kujifunza haya yafuatayo, ikiwa hukuwahi kufayahamu awali.

Katika ufugaji wa kuku, kuna *hasara* na *faida* ambazo zimefichika. Soma na uzingatie yafuatayo;

1] Usiweke kuku pamoja na aina nyingine ya ndege (bata mzinga au khanga) kwa kusudi la kulinda uhuru wao kitabia . Ingawa hakuna athari ya moja kwa moja lakini ikumbukwe kuwa wote wana TABIA tofauti, inayopelekea mmojawapo kukosa uhuru na kuwa *stressed*. Athari yake itaonekana kwenye utagaji mayai haswa wa bata mzinga.




2] Pia haishauriwi kuweka pamoja khanga na kuku, kwani athari yake itaonekana kwenye utagaji mayai haswa wa khanga. Na zaidi haishauriwi kabisa kabisa kuweka Bata Maji karibu na/au pamoja na mifugo mingineyo, kwani usafi wa bata maji ni hatarishi sana kwa kuku na mifugo ya jamii ya ndege.

3] Unapofanya usafi kwenye banda la kuku, epuka kuacha mlundikano wa kinyesi/samadi ndani mwa banda, kwani uvundo wake wenye harufu kali utapelekea athari kwenye mifugo.

4] Epuka vumbi jingi bandani (*contaminated dust*) litakalofanyika kuwa kibebea *(carriers)* cha bacteria au/na virusi vyenye athari kwa afya ya mifugo yako. Epuka kabisa kufanya usafi wa kutimua vumbi ndani ya banda la mifugo yako au kufanya usafi na mifugo ikiwepo bandani.

Kuweza kudhibiti vumbi jingi na vijidudu nyemelezi vya magonjwa kama utitiri, viroboto nk, unashauriwa kunyunyiza dawa mara kwa mara kila ufanyapo usafi bandani.



5] Unashauriwa kufuga Khanga , kwani uzoefu unatuonyesha kuwa Khanga ni wa kuaminika zaidi katika ULINZI (***reliable watchdogs***) wa mabanda yako ya ufugaji. Tabia ya Khanga ni kuonyesha hali ya utulivu kwa wenyeji, lakini pale atakapotokea *mgeni* yeyote (mtu au mnyama hatari) basi Khanga ataashiria kwa sauti ya kelele kali, na pindi *mgeni* huyo anapozidi kusogelea sehemu husika, basi KELELE zitakuwa nyingi kiasi cha kukuamsha hata ukiwa usingizini. Hakikisha kuna mwanga (taa) itakayowawezesha khanga hao kuona ugeni wowote utakaofika.



6] Kinga ni bora kuliko tiba. Mfugaji anawajibika kujifunza kwa habari ya chanjo muhimu za kuwapa mifugo yako. Lakini pia zingatia hili; **Usiwape kuku CHANJO wakati tayari wameonyesha dalili yoyote ya ugonjwa husika. Ukifanya hivyo athari yake itakuwa kubwa**, maana chanjo itapekelekea matokeo hasi badala ya matokeo chanya. EPUKA kwa kuwasiliana na wataalamu wa mifugo eneo la karibu nawe.

7] Kama vile ambavyo KELELE au KUSHTUKA ni mambo yasiyompendeza binadamu yeyote, basi vivyo hivyo jitahidi sana kuzuia USUMBUFU wowote wa MAKELELE au TUKIO LA KUSHTUKIZA kwenye mifugo, haswa kuku wanaotaga mayai. Hii itawapelekea kushtuka '*stress*' itakayoathiri utagaji wa mayai.

8] Ikiwa unafuga makundi ya kuku kwa kutofautisha umri, basi EPUKA kuchanganya vifaranga wadogo na wakubwa mahali pamoja, kwani itasababisha wadogo kudonolewa na kupelekea majeraha, magonjwa na hata vifo.

9] Usiwarundike vifaranga wakubwa au kuku kwenye eneo moja lenye ufinyu wa nafasi. Kuku watakuwa '*stressed*' na kuanza kushambuliana. Mrundikano wa mifugo huongeza gharama za utunzaji na pia ongezeko la vifo kutokana na maambukizi ya magonjwa kama coccidiosis.

10] Usiruhusu UPEPO mkali kuingia kwenye banda la kuku ili kuepuka baadhi ya magonjwa. Vile vile usirihusu MWANGA mkali kuingia kwenye banda.

11] Hakikisha uwepo wa matandazo *safi* muda wote kwenye sakafu ya banda la kuku, kwani kinyesi kilicho wazi si salama kwa afya ya mifugo yako. Ufugaji wa ndani unaathirika sana katika jambo hili.

12] Hakikisha mayai yanaokotwa kila mara (baada ya kila masaa mawili) baada ya kutagwa. Hii itasaidia usafi wa mayai na kuzuia kudonolewa. Hakikisha viota vinadumu katika usafi.

13] Hakikisha kuku wanapatiwa chakula mapema ya *saa 12 asubuhi* kwa siku za kawaida au *saa 11:30 asubuhi* kwa siku ambazo jua linachomoza mapema alfajiri (miezi ya Novemba/Desemba) . Kusudi ni kuwasaidia kuku uwezo wa kutengeneza mayai kwa wakati. Ucheleweshwaji katika kuwapa kuku chakula mapema (mfano saa 2 au 3 asubuhi) hupelekea kuku kuacha kutaga au kupunguza sana kutaga. Wafugaji wengi wameathirika kwa hili, kwani wingi wa kuku haushabihiani na utagaji mayai.



14] Hakikisha UNAFUATILIA KWA MAKINI wastani wa utagaji mayai wa kuku wako. Weka rekodi sahihi ya utagaji mayai siku kwa siku, na wiki kwa wiki. Kujiridhisha katika hili, unaweza kumuweka pembeni kwa muda msimamizi/msaidizi wako katika ufugaji ili uweze kufanya ukaguzi huru wa idadi ya mayai yanayotagwa kwa siku na wiki. Hii itahamasisha nidhamu na uaminifu kwenye mradi wako.

15] Hakikisha mayai yanahifadhiwa kwenye *trays* safi, huku ncha kali ya yai ikielekea chini. Mayai yahifadhiwe kwenye hali ya ubaridi au ndani ya friji yenye ubaridi wa wastani. Kwa mayai ya mbegu kwa ajili ya kutotolesha, epuka mtikisiko mkubwa katika kusafirishwa eneo hadi eneo.



16] Mayai machafu kamwe yasitumike katika utotoleshaji (*incubators*) badala yake yasafishwe kwa maji na yatumike kwa kula. Mayai yaliyosafishwa kwa maji hayafai tena kuangulishwa. EPUKA kutotolesha mayai mengi kipindi cha JOTO kali (miezi ya Novemba/Desemba/Januari) kwani mayai mengi hukosa mbegu kutokana na athari ya JOTO kwa majogoo kushindwa kuwa *machachari* muda mwingi.

17] Hakikisha **vyombo vya chakula havimwagi chakula nje, kutakapopelekea upotevu wa chakula** na ongezeko la gharama za ulishaji. Pia zingatia usafi wa kila siku wa vyombo vya maji, ili kuzuia maambukizo ya magonjwa kupitia vyombo vichafu.



18] Zingatia kuwapatia kuku wako majani ya mbogambona ili kuimarisha afya ya mifugo yako na ubora wa mayai yako. Lakini pia epuka kutumia kemikali ili kutengeneza unjano wa mayai yako.



19] Jifunze kwa kina na uzingatie ratiba ya CHANJO. Kwa maana Chanjo na Usafi ndio msaada mkubwa sana kwa afya ya mifugo yako.

20] Usilazimishe kuwapa chanjo mifugo ambayo ipo kwenye matibabu ya dawa fulani. Utatakiwa kusubiri hadi wamalize dawa ya kutibu ugonjwa husika ndio uendelee na ratiba ya Chanjo. Kumbuka utalazimika kuwapatia mifugo yako VITAMIN (*anti-stress*) ili kuwapatia ahueni kutoka kwenye nguzu za dawa na chanjo.

21] Ikiwa utatumia jiko la mkaa (*kwa ajili ya kuwa chanzo mbadala cha joto kwa vifaranga ikiwa umeme utakatika*) unashauriwa kuhakikisha moto wa mkaa ni mwekundu sana kisha ufunikwe na majivu. Moto wa mkaa usipokuwa mwekundu, mkaa mweusi utaendelea kuwaka na kupekelea gesi hasi kwenye vifaranga.

22] Epuka kuwapa mifugo yako chakula dhaifu, kwani athari zitaanzia tokea wakiwa vifaranga hadi kufikia kuku wanaotaga. Mfugaji anaweza kuathirika na utagaji duni wa mayai ulioanzia kwenye chakula duni walichokula vifaranga hadi kukua kwake, na akaishia kulalamika badala ya kujifunza kutokana na makosa hayo.

23] Epuka kabisa kuku wa mtaani kuingia kwenye eneo la ufugaji wako, kwani kuku wasiotunzwa na panya ni wasambazaji wakubwa wa magonjwa ya kuku.

24] Epuka kabisa kuwapa kuku chakula chenye uvundo au umaji maji. Hakikisha kuku wanapatiwa chakula kikavu, na ikiwa unasafirisha chakula kutoka eneo hadi eneo kipindi cha mvua, zingatia uangalizi na usafiri wa chakula hicho.

25] Zingatia KUIMARISHA KINGA YA MWILI ya *mifugo* yako dhidi ya magonjwa kwa kuimarisha upatikanaji wa CHAKULA BORA na ziada ya VITAMIN na PROTINI pasipo kuwepo athari kwenye uzito wa kuku. Mimea ya kiasili kama ***Aloe-Vera***, ***Mwarobaini***, ***Mlonge*** na ***Lusina*** ni mizuri katika kuimarisha kinga kwa mifugo yako, haswa ukiandaliwa masaa 12 hadi 24 kabla kupewa mifugo.

26] Jiepushe kabisa kuuza mayai au kuku wa nyama kwa matumizi wa wanadamu hali ukijua wazi kuwa mifugo yako imepewa dawa yenye masharti ya zuio la muda *(withdrawal period)* kwa mayai au nyama kutumiwa na wanadamu. **SAYUNI POULTRY Gosheni** **tunakumbusha kwa msisitizo kuwa** **Heshimu utu wa watu*, **Heshimu Afya za watu** * na zaidi *epuka DHAMBI, na laana* katika hilo. UtakavyoTENDA ndiyo vivyo utakavyoTENDEWA hapahapa duniani.

27] Jitahidi kupata '*wasaidizi*' wenye ***nia ya dhati*** katika maendeleo ya mradi wako wa ufugaji. Eneo hili la '*wasaidizi*' lina changamoto kubwa katika maeneo mengi ya ujasiriamali, hivyo usisite kuchukua hatua stahiki dhidi ya '*wasaidizi wasimamizi legelege*'. Na tena epuka kabisa kuendekeza 'ma-*jipu*' kwenye mradi wako, shughulika nao, **wewe binafsi ukiwa mwangalizi na msimamizi mkuu**.

Tunakukaribisha;

SAYUNI POULTRY Gosheni

Mbezi Mwisho, Dar es Salaam | 0712 057514 na 0754 282869 | poultrysayuni@gmail.com

[Mbezi Stand ya Zamani |Eneo la Mbezi Shule |Jirani na Ofisi za Kata/Mashine ya Nafaka]

'the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way'

Kutoka kwetu utapata yafuatayo;

- **VIFARANGA** vya **KUKU - CHOTARA**, ~~**KUROILER**~~, **KENBRO**
- **CHAKULA** cha **MIFUGO** na **VYOMBO** [**feeders & drinkers**] vya **MIFUGO**.
- **KITUO CHA USHAURI** kuhusu **UFUGAJI** na **MAJARIDA bure**,
- **HUDUMA** kwa **WATEJA kwa njia ya simu** [**0777 424 646** muda wa kazi]
- **USAFIRI wa VIFARANGA bure** [NJIA KUU hadi Ubungo, Kibaha, Goba, Maramba Mawili]

'the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way'

SAYUNI POULTRY – GOSHENI tunakujulisha kuwa UFUGAJI wa KUKU wa kienyeji (**CHOTARA**) ni chanzo cha '**WHITE MEAT**' ambayo ni bora zaidi kwa ajili ya afya yako [visit: ***thepoultryguide.com/white-meat-vs-red-meat/***] . Jenga tabia ya kula kilicho BORA kutoka matunda ya kazi yako mwenyewe.

SAYUNI POULTRY – GOSHENI inakupatia kifaranga CHOTARA, KUROILER na KENBRO wa (*umri*) **siku 1-3** kwa bei ya Tzs: **2,000**= [kwa idadi kuanzia box 2 bei ni Tzs: **1,800**= kwa kifaranga] . Tunaweza kumtunzia *Mfugaji* vifaranga hadi wa umri wa siku 10 – 14 kwa makubaliano. Tunakushauri utumie vema **eneo la kiwanja chako** na '**nguvu kazi ya nyumbani kwako**' (house-maids au vijana walio likizo za shule) katika **kuzalisha kipato** zaidi kupitia UFUGAJI na **sio kuzalisha gharama**.[*Effective use of area and human labour as an ASSETs*]



Vifaranga wa LEO ndio kuku wa KESHO; Vijana wa LEO ndio taifa la KESHO; Uwekezaji wa LEO ndio faida ya KESHO. Ni wakati wa kuchukua HATUA sasa; "**UNAWEZA..,tena INAWEZEKANA**" . Unaweza kufuga **kiFamilia** au **kikundi cha Vicoba/ Saccos, umoja wa Wanachuo/ Wafanyakazi**]

Maelekezo muhimu ya awali kwa malezi ya vifaranga vya kuku CHOTARA:

- **Wiki ya KWANZA (siku 1 – 7)**
  Vifaranga wapatiwe chakula "STARTER" na maji masafi yenye 'GLUCOSE' pamoja na Vitamins kwenye maji. Wapatiwe joto kwa njia ya umeme kwa 'BULB' mbili (2) za 100watts, au kwa njia ya jiko la mkaa uliofunikwa na majivu. Watahitaji joto sawia (required heart) kwa masaa 24 ndani ya siku 7.

  Chanjo : katika **Siku ya 7** lazima vifaranga wapatiwe chanjo ya '**Newcastle**' (***kideri /mdondo)*** Ugonjwa huu unaweza kuua vifaranga kwa 50% hadi 100%. Hivyo chanjo ni muhimu sana.

  Changamoto: katika kipindi hiki usafi ni muhimu sana ili kuzuia magonjwa ya kuambukiza. Vifaranga hupenda kula chochote wakionacho ikiwa ni pamoja na kinyesi cha mwenzake, au hata kuachilia kinyesi kwenye maji ya kunywa kitakachoweza achilia magonjwa kwa wengine kwa mfano; typhoid au concidiosis. Katika umri huu vifaranga pia hushambuliwa na 'flu/mafua' ikiwa usafi wa banda hautazingatiwa. Jitahidi kuwasiliana na 'Huduma kwa Wateja' au wataalam wa mifugo kwa msaada zaidi



Banda lako liwe la ukubwa wa 1.5m x 1.5m . Lazima uzingatie usalama wa vifaranga dhidi ya panya, paka au vicheche. Unatakiwa kuweka 'maranda ya mbao' chini kwenye sakafu yatakayosaidia usafi. Hakikisha usafi unafanyika mara kwa mara, na pia zingatia sana chanjo.

- **Wiki ya PILI (siku 8-14)**



Vifaranga wataendelea kupewa chakula "STARTER" na maji yenye Vitamin na chanzo cha mwangaza (lights) muda wote, lakini si lazima sana kupewa nyongeza ya joto, labda ikilazimika kutokana na hali ya hewa ya eneo husika.

Chanjo :katika **Siku ya 14** lazima wapewe chanjo ya "**gumboro**"kwenye maji ya kunywa.

- **Wiki ya TATU (siku 15-21)**

Vifaranga wataonyesha kuchangamka zaidi, na uhitaji wa joto utapungua, ila ni kipindi ambacho wanakula chakula zaidi kwa ajili ya kukua. Ni vizuri waendelee kupata taa ili kupata mwangaza utakayowawezesha kula mchana na usiku.

Chanjo :katika **Siku ya 21** lazima **warudie** chanjo ya "**Newcastle** (aina ya IBDL)".

- **Wiki ya NNE (siku 22-28)**

Chanjo :katika **Siku ya 28** lazima **warudie** chanjo ya "**gumboro** (aina ya IBDL)".

RATIBA YA CHANJO

UMRI - Siku/wiki	Aina ya chanjo	Njia ya kuwapa
siku 1 – 5	Glucose ,	Maji ya kunywa
	"OTC +" na "Typhoprim"	Maji ya kunywa
Siku 7	NewCastle	Maji ya kunywa
Siku 14	Gumboro	Maji ya kunywa
Siku 21	NewCastle **(IBDL)	Maji ya kunywa
Siku 28	Gumboro **(IBDL)	Maji ya kunywa
Miezi 2 (wiki ya 8)	Ndui	Sindano
Miezi 2	Minyoo	Maji ya kunywa

- Wiki ya 8 tenga Vijogoo na Vitetea. Wape vijogoo chakula cha kunenepesha.
- Wiku ya 16 kata kuku midomo na undae viota.
- Rudia chanjo ya NewCastle na minyoo kila baada ya miezi 3



SAYUNI POULTRY – GOSHENI pia ni wafugaji na wauzaji wa **Bata Mzinga, Khanga** na **Kware** ambao nao wana soko zuri. Pia wanafaa sana kwa ajili ya "**Nyama Choma**" ya nyumbani pamoja na familia yako au ukipata wageni [Home BBQ recreations] Hii ni fursa ya kuthubutu na kuchukua hatua.



SAYUNI POULTRY Gosheni - tunasema "**UNAWEZA..,tena INAWEZEKANA**". Wasiliana nasi kwa;

+255 712 057 514

+255 754 282 869

sayunipoultrygosheni.blogspot.com

'the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way the life the truth the way'